Maagizo Ya Daktari

na

Ellis P. Forsman

Maagizo Ya Daktari

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 7, 2011

Maagizo Ya Daktari

Math. 9:12

Je umewahi kuwa mgonjwa na ukalazimika kumwita tabibu? Je siku nyingine hujawai kusema, “Hayo ni maagizo ya daktari”?

Watu wachache hawajawai kumtembelea daktari kwa sababu ya ugonjwa. Maelfu ya watu kila siku wanajaribu kufuata maelekezo ya daktari, kwa sababu wanajua maisha yao yanategeme tiba.

Labda, agizo likawa ni upasuaji ili kuepuka kifo. Au labda, daktari ameagiza madawa maalum ambayo inamanisha kufa na kupona. Wakati mwingine mgonjwa anajibu, “Ni heri kufa kuliko kufuata agizo la daktari,” wakati agizo linaonekana halimpendezi.

Watu wengi watapendekeza kufuata agizo la daktari kila wakati, bila kujali kutokuwa na hamu ya kumeza dawa, au gharama yake, kwa sababu bado ni bora kuliko madhara ya kutokufuata maagizo ya daktari.

Leo, ulimwengu unaumwa. Nafsi za wanadamu zinaumwa kwa sababu ya ugonjwa unaoua wa dhambi.

Pigo la dhambi

Wakati wa agano la kale, neno “pigo” maranyingi ilikuwa inatumika katika ugonjwa wa ukoma. Katika nyakati hizi neno hili linatumika katika madhara na ugonjwa unaouwa.

Ugonjwa mbaya unaouwa kati ya magonjwa yote ni dhambi, pigo la moyo. Kumbukumbu imefanywa kuhusu dhambi kama pigo katika 1 Wafalme 8:38.

1 Wafal. 8:38, *“Maombi yoyote au dua yoyote ikifanywa na mtu awaye yote, au na watu wako Israeli wote pamoja, watakaojua kila mtu maradhi ya moyo wake, na kuikunjua mikono yake kuielekea nyumba hii.”*

Tangu mwanzo wa bustani ya Edeni pigo la dhambi limekuwa likitenganisha sana. Eva alishikwa na pigo la dhambi, na Adamu naye akaambukizwa naye. Kwa hiyo, kijana wao wa kwanza akamuua kaka yake.

Ogonjwa mbaya ukaendelea tokea mwanadamu aanze kuijaza nchi.

Na Mungu akakagua mazingira ya mwanadamu na akasema:

Mwanzo 6:5-6, *“BWANA akaona ya kuwa maovu ya wanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni*

baya tu sikuzote. BWANA akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo."

Paulo ana sisitiza umaana wa pigo la dhambi alipoandika kwamba wanadamu "*walikuwa chini ya dhambi....":*

Waru. 3:9-18, *"Ni nini basi? Tu bora kuliko wengine? La! Hatakidogo. Kwa maana tumekwisha kushitaki Wayahudi na Wayunani ya kwamba wamekuwa chini ya dhambi; kama ilivyoandikwa, ya kwamba, hakuna mwenye haki hata mmoja. Hakuna afahamuye, hakuna amtafutaye Mungu. Wote wamepotoka wameoza wote pia; hakuna mtenda mema la" hata mmoja. Koo lao ni kaburi wazi, kwa ndimi zao wametumia hila. Sumu ya fira i chini ya midomo yao. Vinywa vyao vimejaa laana na uchungu. Miguu yao ina mbio kumwaga damu. Uharibifu wa masha yamo njiani mwao. Wala njia ya amani hawakuijua. Kumcha Mungu hakumo machoni pao."*

Ni nini kilichopo dhidi ya mwanadamu! Ni maelezo gani mabaya yanayoleteleza pigo la dhambi.

Kila nafsi ya mwanadamu imeathiriwa na ugonjwa mbaya wa dhambi.

Madhara Dhambi

Madhara ya dhambi yanaweza yakawa ya kufisha.

Dhambi inapukutisha akili, inapukutisha mwili, na itaangamiza nafsi ya mwanadamu. Inapukutisha mji, inapukutisha jamii, na inaweza kuangamiza taifa. Inatafuna kama kansa iliyoko katika nafsi ya mwanadamu. Dambi inachana, alafu inadhoofisha. Mshahara wake ni mauti.

Waru. 6:23*, "Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele kupitia Yesu Kristo Bwana wetu.*

Hebu tukumbuke maneno ya Paulo kwa Wagalatia, Wagal. 6:7-8, "*Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi: kwa maana kile apandacho mwanadamu ndicho atakachovuna. Kwa maana yeye apandaye katika mwili atavuna vya mwili; bali yeye apandaye katika Roho kwa Roho atavuna uzima wa milele."*

Dhambi haitibiki kupitia wakala waMwanadamu

Hakuna mwanadamu awezaye kujitibu mwenyewe kutoka na ugonjwa huu wa dhambi. Sababu ya kibinadamu, kwa kupingana na imani, imejaribu na ikashindwa.

Wote wasiomwamini Mungu, wasiojua kwamba Mungu yuko, na wasiojua chochote katika ulimwengu wameshindwa kutoa msaada kwa mwenye dhambi anayeumwa nafsi. Mfumo wa wanadamu wa kidini umejaribu ukashindwa. Mwanadamu, mwenyewe, alikuwa tayari kurejesha hata pigo moja la nafsi uliovunjika.

Dawa ya daktari mkuu

Kuna dawa ya pigo hili. Kuna tiba, kama tukifuata maelekezo ya daktari.

Dawa haijaonyeshwa kwa mtindo wa kujionyesha mtaani, au kwa amri ya wanadamu. Dawa inatoka kwa tabibu mmoja ambaye anaweza kutoa idhini ambayo itatibu ugonjwa ulioko katika nafsi ya mtu. Tabibu huyo ni Tabibu Mkuu, Yesu Kristo, mwana wa Mungu, ambaye wakati fulani alisema:

Math. 9:12, *"...Wenye afya hawaitaji tabibu, bali waliohawawezi."*

Sifa za tabibu

Kama mwana familia wetu atakuwa mgonjwa mahututi – amepigwa na ugonjwa unaouwa – hakika tutatafuta huduma kwa daktari mwenye ujuzi na sifa, na tuta lazimika kufuata masharti ya tabibu.

Siyokawaida kwa wanadamu kusafiri maelfu ya maili na kutumia muda katika pesa ili tu aokowe ugonjwa wa mwili, au kuwa na maisha mazuri katika mwili kwa muda mfupi uliopita.

Chini ya mazingira kama hayo, mgonjwa anatakiwa kufuata maelekezo ya daktari katika kila dakika.

Hataivyo, kutoa uhai wa mtu katika mikono ya tabibu wake, mwanadamu lazima ajue sifa za tabibu huyu. Imeshawai kutokea katika matibabu ya ugonjwa wako? Ni mafanikio gani yaliyopo katika sehemu hii?

Nafsi inayoumwa inaweza kutibiwa kabisa kama tutamwachia mwenyewe afuate maagizo ya daktari kwa uthabiti.

Kwa bahati mbaya, watu wengi ambao ni wagonjwa, wanakata tama hadi kufa, wakifikiri ni wazima na hawana itaji la tabibu.

Hawatasema pigo lilopo katika mioyo yao.

Wengine wanaweza kusema kwamba wao wanaugonjwa wa dhambi, na kuhitimisha kuwa ugonjwa wao si mbaya sana, kwa hiyo hawaungi mkono swala hili la kufuata Tabibu Mkuu. Mamilioni ya wenye dhambi wanakufa bila kujitayarisha kukutana na Mungu kwa sababu ya utofauti.

Agizo la tabibu limepotoshwa

Leo, nafsi nyingi zenye dhambi zinazoumwa wamechanganyikiwa kutoka na hitaji lao la Tabibu Mkuu, na wanahitaji wamuone kuhusiana na hali yao na matibabu, lakini hawana imani iliyokamilika katika yeye.

Maranyingi hawako tayari kufuata maagizo ya tabibu. Hakuna mtu anayeweza kupoteza nafsi yake kwa sababu ya kubadilisha agizo la daktari.

Katika mpango wa Mungu wa wokovu, sawa na kwenye dawa, mwanadamu hawezi kuchezea agizo la daktari! Kuzidisha au kupunguza maelekezo ya daktari haijawai kufanywa na wauza madawa waliohitimu. Sheria ya inchi inakinga miili yetu na watu wasio elimu ambao wanaweza kuchezea maagizo ya daktari, lakini ni juu ya kila mmoja kuona kwamba kila msingi uliotolewa na Tabibu Mkuu unafuatwa bila kuzidisha au kupunguza.

Hili ni swala linalohusu hatima ya nafsi ya mwanadamu. Madhara ni mabaya sana.

2 Yoh. 1:9, *"Kila apitaye cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia."*

Ni ukweli unaojulikana kwamba madawa Fulani yanaweza kutumika ili kukidhi uzima katika mwili; na madawa hayo ayo yanayotumika vibaya katika mikono ya wasio na elimu na ufahamu wanaweza kusababisha kifo.

Injili ya Kristo, ambayo ndiyo agizo lililovuviwa la Tabibu Mkuu, ni uwezo wa Mungu kuokowa anayeamini.

Waru. 1:16, *"Kwa maana siionei haya injili. Kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye , kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia."*

Lakini injili iliyopotoshwa, ambayo wanadamu wameipotosha, inaweza kumaanisha kufa kiroho tu.

Wagal. 1: 7-8, *"Wala si nyingine lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe."*

Hatua za usalama

Kila mhubiri lazima awe wazi kwamba anakiri na kufuata maelekezo kama ilivyotolewa na Tabibu Mkuu. Kila mtu na ajue kwamba agizo la daktari isichezewe.

Lazima tuchunguze kwa makini dawa yoyote ya kiroho inayotolewa na mwalimu ye yote wa kidini.

1 Yoh. 4:1, *"Wapenzi msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu, kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani."*

Kila mtu lazima achunguze na kuona kama waalimu wa kidini wanatoa mafundisho sawa na jinsi Tabibu Mkuu alivyoagiza. Kila mtu anapaswa kuwa makini na mtu ye yote anayeweza kusema, Najua Biblia inasema ivyo, "lakini sidhani kama ni mhimu."

Chunguza maandiko kama imenukuliwa vibaya au imetumika vibaya. Kama mtu hana tatizo na kubadilisha agizo la daktari, itakuwa kwamba nafsi hiyo itakuwa pabaya. Kumbuka ni nafsi yako ndioinatakiwa iokolewe au ipotee.

Kukataa hakuna udhuru

Kukataa hakuta mtibu mgongwa kutokana na mdhara ya ugonjwa, hata kifo, wakati maagizo ya daktari yanapofuatwa. Ukataaji upande wa mgonjwa hakuna tiba kutoka katika madhara ya kuuwa.

Baadhi ya walimu wa dini wanaweza wakayakataa maandiko, wengine wanaweza wasijali au waaminifu. Majibu yote ni sahihi – kosa ambalo haliwezi kubadilishwa milele!

Mtu ambaye anaweza kunywa sumu inayouwa kupitia kosa, wuenda kosa au sehemu ya mnywaji. Au kila mmoj ambaye agizo lilitolewa, anaweza akawa amekufa utafiri alipanga kujiuwa.

Haifanyi tofauti kile ambacho mtu anaamini. Bado tu atakufa.

Tahadhari

Faida ya kudanganywa inaweza kuwa hasara ya nafsi katika umilele. Onyo imetolewa wazi muda mrefu na Tabibu mkuu katika Biblia:

- Waef. 5:6, *"Mtu asiwadanganye kwa maneno yasiyo na maana; kwa kuwa kwa sababu ya hayo asira ya Mungu huwajia wana wa uasi."*

- Math. 15: 9, *"Wananiabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyomaagizo ya wanadamu."*
- Math. 15: 13-14, *"Akajibu akasema kila pando asilolipanda Baba yangu wa mbinguni litang'olewa. Waacheni hao ni viongozi vipofu wa vipofu. Na kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, watatumbukia shimoni wote wawili."*
- Wakol. 2:8, *"Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu, wala si kwa jinsi ya Kristo."*

Agizo la tabibu

Naomba niwawakilishie agizo la daktari kwa kila nafsi yenye dhambi inayoumwa. Hautakosea ukifuata maelekezo ya Tabibu Mkuu.

Utapotea katika umilele kama hufuati maelekezo yake.

Lazima uamini.

- Waeb. 11:6, *"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpndeza, kwa maana mtu amuendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao."*
- Yoh. 8:24, *"Kwa hiyo naliwaambieni kwamba mtakufa katika dhambi zenu; kwa sababu msiposadiki ya kuwa mimi ndiye, mtakufa katika dhambi zenu."*

Tahathari: kuwa makini katika maagizo ya daktari, au ufe.

Lazima utubu.

- Luka 13:3,5, *"Nwaambia sivyo, lakini msipotubu ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo. Nawaambia sivyo lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo."*
- Matend. 17:30, *"Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni, bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu."*

Lazima umkiri Kristo.

- Matend. 8:37, *"Filipo akamwambia ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana. Akajibu akasema, naamini ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu."*

- Math. 10:32, *"Yeyo atakayenikiri mbele za watu name nitamkiri mbele ya Baba yangu aliye mbinguni."*

Kumbaka: Angalizo la tabibu, au uponyaji unakataliwa.

Lazima ubatizwe – kuzikwa ndani ya maji.

- Marko. 16:16, *"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."*
- Matend. 2:38, *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*
- Matend. 22:16, *"Basi sasa unakawilia nini? Simama ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake."*

Ubatizo mara nyingi unawekwa katika mpango wa Mungu uliotolewa na Tabibu Mkuu.

Mwisho

Hakuna mtu, kikundi cha watu walio na haki au mamlaka ya kubadilisha, kupindua au kugawanya katika mpango mzima wa kuokolewa kwa mwanadamu.

Vile vile, siyo kawaida kwa watu leo, wanaodai kwamba wameitwa na Mungu kuhubiri neno lake, kuondoa kabisa, kuboresha, na kuondoa katika mpango wa Mungu wa kuondoa dhambi.

Lazima kwa makini tuzingatie maelekezo yaliyotolewa na Tabibu Mkuu.

- Math. 28:20, *"Na kuwaa fundisha kushika yote niliyowaamuru ninyi, na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."*
- Yoh. 4:24, *"Mungu ni Roho; na wao wamwabuduo imewapasa kumuabudu katika roho na kweli."*
- 2 Yoh. 1:9, *"Kila apitaye cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia."*
- Wakol. 3:17, *"Na kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye."*

- 1 Petr. 4:11, *"Mtu akisema na aseme kama mausia ya Mungu, mtu akihudumu na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu, ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele. Amina."*

Maelezo yaliyovuviwa ni rahisi na yanaeleweka kiurahisi. Ni agizo la mbinguni tu ndilo kamili na nithabiti kutibu nafsi yenye dhambi ya mtu.